# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

**HOTUBA YA MGENI RASMI**
**DK. SALIM AHMED SALIM**
**MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE**

**CHAKULA CHA JIONI KILICHOANDALIWA NA**
**TARENA MKOA WA DAR ES SALAAM**

**28 APRILI 2003**

**KUCHANGIA FEDHA ZA MAANDALIZI YA KONGAMANO LA**
**WAUGUZI SIKU YA WAUGUZI DUNIANI**

**HOTUBA YA DK. SALIM AHMED SALIM,**
**MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE**
**KWENYE CHAKULA CHA JIONI KILICHOANDALIWA NA**
**TARENA MKOA WA DAR ES SALAAM**
**KUCHANGIA FEDHA ZA MAANDALIZI YA KONGAMANO LA**
**WAUGUZI SIKU YA WAUGUZI DUNIANI**

- Mwenyekiti wa TARENA, Mama Anna Ngelime;
- Muuguzi Mkuu wa Serikali, Mama Joyce Safe;
- Viongozi Wote wa TARENA;
- Wageni Waalikwa;
- Mabibi na Mabwana.

Kwanza ninapenda kuungana na Mwenyekiti wa TARENA Mkoa wa Dar es Salaam kuwakaribisha waalikwa wote mliohudhuria hapa. Madhumuni ya chakula hiki ni kuchangia gharama za maandalizi ya "Kongamano la Kuboresha Huduma za Uuguzi kwa Wagonjwa" litakalofanyika wakati wa Kuadhimisha Siku ya Wauguzi Duniani. Hii huadhimishwa tarehe 12 Mei kila mwaka. Kwa niaba yenu

wote ninaomba kuwashukuru viongozi wa TARENA kwa ukarimu wao wa kutualika kuja kwenye chakula hiki cha jioni hivi leo.

Ninapenda pia nitoe shukrani zangu binafsi kwa kunialika kuja hapa leo na kuwa Mgeni Rasmi. Hii ni heshima kubwa kwangu mimi binafsi na pia kwa Taasisi ya Mwalimu Nyerere ambayo mimi ni Mwenyekiti wake wa Bodi ya Wadhamini.

Nimeelezwa kuwa kila mwaka madhimisho ya "Siku ya Wauguzi Duniani" huambatana na kaulimbiu iliyoandaliwa. Kwa mwaka huu (2003) Kaulimbiu ni "*Wauguzi Katika Mapambano Dhidi ya Unyanyapaaji wa Wagonjwa wa Ukimwi na Kutoa Huduma kwa Wote.*" Ninaamini kuwa kaulimbiu hii imekuja wakati mwafaka hasa kwa kuzingatia

athari ya ugonjwa wa ukimwi kwa maisha ya Watanzania na kwa uchumi wa Taifa letu kwa jumla. Watanzania wote tunajua jinsi ugonjwa wa ukimwi unavyoua watu wetu. Wote tunajua jinsi vijana wetu ambao ndio nguvu kazi yetu wanavyopoteza maisha yao kutokana na UKIMWI. Kasi ya maambukizi, kuumwa na vifo vinavyotokana na ukimwi ni kubwa sana. Ni ukweli uliowazi kuwa familia nyingi hapa Tanzania zimeathirika na ukimwi kwa njia moja au nyingine. Sote tunajua kuwa siku hizi haipiti siku bila kusikia taarifa za vifo ambavyo vinatokana na ukimwi au kuwaona wagonjwa wa ukimwi. Ingawa matangazo ya hadhara hayasemi huyu kafa kwa ukimwi au yule amelazwa na anaugua ukimwi lakini ukweli ni kwamba hiyo ndio hali halisi.

Hapa ningependa kunukuu yale niliyoyasema Iringa tarehe 1 Desemba 2002 katika Maadhimisho ya Kitaifa ya

Siku ya Ukimwi Duniani: "... *Kwa muda mrefu, kwa baadhi yetu, na pengine kwa wengi wetu, iliaminika kwamba ukimwi ni janga lililo mbali nasi binafsi; ambalo linaweza kumpata ndugu mwingine, rafiki au jirani. Ni kweli, tunasikitika na kusononeka tukiwaona wengine, lakini baadae tunasahau. Lakini. Katika hali tuliofikia hivi sasa, imejitokeza wazi kwamba dhana hiyo sio sahihi hata kidogo. Wale wenye virusi, wale wenye magonjwa yanayotokana na virusi hivyo, pamoja na wale wasiokuwa navyo, wote tumekuwa waathirika. Ndugu zangu, hali ilivyo hivi sasa, ni kwamba baadhi wameambukizwa lakini wote tumeathirika na janga hili. Hali halisi pia ni kwamba karibu kila mmoja wetu hapa ameguswa; aidha ameuguza au amezika mtoto, mzazi, ndugu, jirani, rafiki au mfanyakazi mwenzake, au ameachiwa watoto yatima."*

Baada ya kuweka wazi hali hii ya kutisha katika nchi yetu na ambayo ni hali inayoathiri sana bara letu kwa jumla, sasa ninaomba nirejee kwenye kaulimbiu ya mwaka huu: "*Wauguzi Katika Mapambano Dhidi ya Unyanyapaaji wa Wagonjwa wenye Ukimwi na Kutoa Huduma kwa Wote.*" Kwa maneno mengine kaulimbiu hii inasema kuwa "**Wauguzi Katika Mapambano Dhidi ya Tabia ya Kuwatenga, Kuwaepuka au Kuwanyanyasa Wagonjwa wa Ukimwi**." Ni muhimu kusisitiza kuwa tatizo la kuwatenga na kuwanyanyasa wagonjwa wa ukimwi ni tatizo la kweli. Ni tatizo ambalo wengi tunalionea haya na wala halizungumzwi ipasavyo. Wataalam wa saikolojia ya tabia ya wagonjwa wanatuambia kuwa unyanyapaaji au tabia ya kuwatenga wagonjwa wa ukimwi inachangia sana kuueneza ukimwi kwa sababu zifuatazo. Kwanza wagonjwa hawajitokezi wazi wazi na kupata ushauri nasaha

utakaowawezesha kuishi na virusi vya ukimwi katika hali ya kawaida. Pili wagonjwa hao kwa sababu hawajulikani na jamii hufanya vitendo ambavyo vinaweza kueneza ukimwi, maana jamii haichukui tahadhari za msingi kuepuka maambukizi kutoka kwa waathirika hao. Ninapenda kusisitiza hapa kuwa tahadhari hizo za kujikinga na maambukizi kutoka kwa waathirika si unyanyapaaji, kuwaepuka au kuwanyanyapaa waathirika bali ni kuepukana na vitendo vile ambavyo vinasababisha maambukizi ya ukimwi.

Kwa kuzingatia kuwa tatizo la ukimwi linahusu uhai wa binadamu wote (na nchi zetu za Afrika zikiwa zinazoongoza kwa maambukizi ya ukimwi kwani katika idadi ya kiasi ya watu milioni 40 walioambukizwa duniani, karibu robo tatu ni Waafrika), ni vyema tukaichukulia kaulimbiu ya Siku ya

Wauguzi Duniani ya mwaka huu kama ni nafasi na changamoto kwa Dunia, ikiwemo nchi yetu ya Tanzania ya kuongeza jitihada za kupambana na ukimwi. Kaulimbiu hii ya "Wauguzi Katika Mapambano Dhidi ya Unyanyapaaji wa Wagonjwa wa Ukimwi na Kutoa Huduma kwa Wote" haina budi kupata tafsiri pana zaidi itakayowahusisha Viongozi wote wa Serikali, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Taasisi ambazo si za Kiserikali, Viongozi wa Taasisi mbali mbali za Kijamii, Watu wa Sekta Binafsi na Watanzania wote kwa jumla. Tukitaka kupata mafanikio makubwa katika vita dhidi ya ukimwi ni lazima jamii ya Watanzania na Viongozi wetu washiriki kikamilifu. Haiwezekani vita na mapambano dhidi ya unyanyapaaji wa wagonjwa wa ukimwi wakaachiwa wauguzi na waganga wengine peke yao. Ni kweli kuwa katika vita na mapambano dhidi ya magonjwa na maradhi waganga katika ujumla wao

tunawatazamia wawe mstari wa mbele lakini kimsingi ni vita vinavyotuhusu sote. Waganga – yaani madaktari, wauguzi na kadhalika wanaweza tu kuwa wapiganaji wa mstari wa mbele lakini Watanzania wote hawana budi kuwa wapiganaji. Hapo hapo napenda kusisitiza kwamba ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kumhudumia mgonjwa wa Ukimwi na kuzuia unyanyapaaji miongoni mwenu katika kutoka huduma hizo. Ni muhimu vitendea kazi muhimu vitolewe kwa wauguzi na wote wahusika.

Bila ya kuchukua muda wenu zaidi nataka nirudi kwa waalikwa wote waliopo hapa leo na wale walioalikwa na ambao hawakupata nafasi ya kufika. Tumekuja hapa leo kwenye chakula cha jioni ili kuchangia gharama za Kongamano ambalo litajadili pamoja na mambo mengine "Jinsi ya Kuboresha Huduma za Uuguzi kwa Wagonjwa" na

pia kaulimbiu au mada inayohusu "Wauguzi Katika Mapambano Dhidi ya Unyanyapaaji wa Wagonjwa wa Ukimwi na Kutoa Huduma." Kwanza nawashukuru wote waliotoa michango yao kwa ukarimu wao. Pili, ninawaomba wasiotoa watoe na waliotoa wakiweza waongeze michango yao leo. Ninatoa wito huu kwa sababu kufanikiwa kwa Kongamano hilo kutasaidia sana kufanikisha vita dhidi ya ukimwi ambao athari zake nimekwishaeleza. Kutafanikisha pia utoaji huduma bora kwa wagonjwa wote. Katika hili wajibu wa wajumbe wa Kongamano ni kujadili na kuweka mikakati ya kutekeleza kaulimbiu ya mwaka huu pamoja na jinsi ya kuboresha huduma kwa wagonjwa. Na wajibu wetu ni kusaidia kufanyika kwa Kongamano hilo.

Naomba kurudia. Vita dhidi ya ukimwi ni ya sisi sote. Ukimwi ni tishio kwa kila mmoja wetu. Ukimwi ni tishio kwa

kila familia; ukimwi ni tishio kwa Tanzania; ukimwi ni tishio kwa Afrika; ukimwi ni tishio kwa Dunia. Ni wajibu wetu wote kupambana na ukimwi. Ukimwi unaweza kupungua na hatimaye kutoweka kama kila mmoja atashiriki katika mapambano ya kuutokomeza. Huduma bora za uuguzi kwa wagonjwa ni muhimu katika kufanikisha tiba kwa wagonjwa wetu. Kuichangia Kongamano ya kuboresha Huduma kwa Wagonjwa ni namna moja ya kuinua kiwango cha tiba na huduma kwa wagonjwa katika nchi yetu.

Asanteni sana.